# MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 02/03/2022

MAHUDHURIO:

1. Bw. Fredrick K. Juma - Mwenyekiti
2. Bw. Damian Morice Ogila - Katibu
3. Bw. Patrice M. Boniphace - Mjumbe
4. Bi. Monica Magutu - Mjumbe
5. Bw. Haruna Matata - Mwanasheria

L.F

WAJUMBE WASIOHUDHURIA:

Bw. Charles Moremi

Bw. Belton Garigo

SEKRETARIETI:

1. Maria P.Machugu – Afisa Ugavi
2. Boniphace Yohana – Afisa Ugavi

AJENDA

1.Kufungua kikao

2.Kupitia na kuthibitisha ajenda

3.Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita cha tarehe 20/01/2022

4.Kujadili na kuidhinisha Ujenzi wa jengo la Dharura Hospitali ya Wilaya Tarime kwa njia ya Force Account

5.Kujadili na kuidhinisha Manunuzi ya vifaa vya kufyatulia beacon (beacon mould) idara ya Ardhi.

6.Kujadili na kuidhinisha Manunuzi ya Mashine1 ya Fotokopi,Kompyuta 3 na karatasi ream 10 Idara ya Ardhi.

7.Kujadili na kuidhinisha Manunuzi ya Mabati 568 ya ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa ya shule na Zahanati 2 kwa fedha za mapato ya ndani idara ya Mipango.

Scanned with CamScanner

8.Kujadili na kuidhinisha manunuzi ya Mashine ya kupima ardhi (RTK machine)idara ya Ardhi.

9.Kujadili na Kuidhinisha Manunuzi ya Huduma ya usafirishaji Mashine ya kufyatulia matofali ya Block kutoka Dodoma hadi Tarime Mji- Idara ya Mipango.

10.Kujadili na kuidhinisha manunuzi ya vifaa tiba vilivyokosekana MSD

11.Kujadili na kuidhinisha Ununuzi wa Dizeli lita 2000 Idara ya Mipango kwa ajili ya ufuatiliaji miradi ya maendeleo

12.Kujadili na kuidhinisha Manunuzi ya matairi 5 Idara ya Afya kwa ajili ya gari la wagonjwa (Ambulance)

13.Kufunga kikao

**MUH NA. HMT/BZ/02/03/2022/01: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni alifungua kikao mnamo saa 4:00 Asubuhi Kwa kuwakaribisha wajumbe.

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/02: KUPITIA NA KUTHIBITISHA AJENDA**

Ajenda zilipitiwa na kuthibitishwa kwa ajili ya kujadiliwa

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/03: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 20/01/2022**

Muhtasari wa kikao cha tarehe 20/01/2022 ulisomwa na katibu na kisha wajumbe waliridhia na kuuthibitisha.

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/04:KUJADILI NA KUIDHINISHA UJENZI WA JENGO LA DHARURA HOSPITALI YA WILAYA TARIME KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT**

Katibu wa bodi ya zabuni aliwasomea wajumbe barua yenye Kumb Na.AH.161/298/01 ya tarehe 13/01/2022 kutoka kwa Kaimu Katibu Mkuu TAMISEMI iliyoelekeza Halmashauri kutumia njia ya Force Account kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya huduma za dharura baada ya kukosekana mzabuni mwenye sifa kwa njia ya Zabuni kitaifa.

AZIMIO: Wajumbe waliidhinisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la dharura kwa njia ya Force Account

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/05: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA VIFAA VYA KUFYATULIA BEACON (BEACON MOULD) IDARA YA ARDHI.**

Katibu wa bodi aliwajulisha wajumbe kuhusu maombi ya idara ya ardhi ya kununuliwa vifaa vya kufyatulia beacon.Nukuu zifuatazo za bei ya wazabuni zilipatikana:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | BEI YA MZABUNI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Andrew Marwa Ketang'enyi | 2,500,000 |
| 2 | Philemon C.Ologi | 3,250,000 |

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Jeremia Ryoba Welding | 3,100,000 |

AZIMIO: Wajumbe wa bodi waliidhinisha mzabuni Andrew Marwa Ketang'enyi kutengeneza vifaa hivyo kwa bei ya Tzs.2, 500,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/06: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA MASHINE1 YA FOTOKOPI, KOMPYUTA 3 NA KARATASI REAM 10 IDARA YA ARDHI.**

Idara ya Ardhi iliwasilisha maombi ya kununuliwa mashine 1 ya Fotokopi, Kompyuta 3 na karatasi Ream 10.Wazabuni wafuatao walijaza nukuu za bei:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | BEI YA MZABUNI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Bismark Rock Computers | 12,200,000 |
| 2 | Princes Business Centre | 12,270,000 |
| 3 | Business Softcom Ltd | 12,620,000 |
| 4 | Caroline M. Stationery | 15,900,000 |

Wajumbe walipitia nukuu hizo za bei na kutoa azimio

AZIMIO: Wajumbe waliidhinisha mzabuni Bismark Rock Computers kuiuzia Halmashauri vifaa hivyo kwa gharama ya TZS.12, 200,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/07: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA MABATI 568 YA UJENZI WA VYUMBA 5 VYA MADARASA YA SHULE NA ZAHANATI 2 KWA FEDHA ZA MAPATO YA NDANI IDARA YA MIPANGO.**

Katibu wa Bodi aliwajulisha wajumbe kuhusu maombi ya idara ya Mipango ya kufanyika manunuzi ya mabati kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ili kujenga Madarasa na Zahanati.

Nukuu za bei zilitolewa na kujazwa na Wazabuni kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | BEI YA MZABUNI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Jura (T) Ltd | 27,736,000 |
| 2 | Chrispinus M.Mukohi | 29,110,000 |
| 3 | Mamaleah Hardware | 29,472,000 |
| 4 | Waja General Co. Ltd | Hakujaza bei ya vifaa vyote |

Wajumbe walijadili nukuu za Wazabuni hao na kutoa azimio

AZIMIO:Wajumbe waliidhinisha mzabuni Jura Tanzania Ltd kuiuzia Halmashauri mabati hayo kwa gharama ya TZS.27,736,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/08: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA MASHINE YA KUPIMA ARDHI (RTK MACHINE) YA IDARA YA ARDHI.**

Katibu aliwajulisha wajumbe kuhusu maombi kutoka idara ya Ardhi ya kufanyika manunuzi ya mashine ya kupima ardhi (RTK machine). Nukuu za bei ilifanyika kwa wazabuni kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | BEI YA MZABUNI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | SURVEX Limited | 26,500,000 |

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Surveying Equipment Services Centre (EA) Ltd | 26,700,000 |
| 3 | Gobal Survey Company Ltd | 32,000,000 |

Wajumbe wa bodi walijadili nukuu hizo za wazabuni na kutoa azimio

AZIMIO: Wajumbe waliidhinisha Mzabuni SURVEX Ltd kuiuzia Halmashauri mashine ya kupima ardhi yenye gharama ya TZS 26,500,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/09: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA HUDUMA YA USAFIRISHAJI MASHINE YA KUFYATULIA MATOFALI YA BLOCK KUTOKA DODOMA HADI TARIME MJI- IDARA YA MIPANGO**

Nukuu ya bei ilipatikana toka kwa msafirishaji (Stephen I. Mushi) mwenye lori lenye mashine ya kupakia na kushusha mizigo (crane) kwa gharama ya Tzs 2,900,000

Wajumbe walijadili namna ya usafirishaji wa mashine hiyo na kutoa uamuzi

Mju

AZIMIO: Wajumbe waliidhinisha Msafirishaji/Transporter Stephen I. Mushi kupewa kazi ya kusafirisha mashine ya kufyatua matofali kutoka Dodoma hadi Tarime kwa gharama ya Tzs 2,900,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/10:KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA VIFAA TIBA VILIVYOKOSEKANA MSD**

Wajumbe wa Bodi walijulishwa kuhusu maombi ya idara ya Afya ya kununuliwa vifaa tiba vilivyokosekana MSD. Baada ya kutolewa nukuu za bei, Wazabuni walijaza bei kama ifuatvyo:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | BEI YA MZABUNI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Kayonza Pharmacy | 4,250,000 |
| 2 | Lubajo Pharmacy | 5,000,000 |
| 3 | Tarime Pharmacy | 6,000,000 |

Wajumbe walijadili nukuu hizo za bei na kutoa uamuzi kuwa Kayonza Pharmacy apewe zabuni ya kuiuzia Halmashauri vifaa tiba vyenye thamani ya Tzs.4,250,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/11:KUJADILI NA KUIDHINISHA UNUNUZI WA DIZELI LITA 2000 IDARA YA MIPANGO KWA AJILI YA UFUATILIAJI MIRADI YA MAENDELEO**

Wajumbe wa Bodi walijulishwa kuhusu ombi la idara ya Mipango ya kununuliwa mafuta ya dizeli lita 2000 kwa ajili ya ufuatiliaji miradi ya maendeleo.Baada ya majadiliano wajumbe waliidhinisha ununuzi wa dizeli lita 2000 yenye thamani ya Tzs 5,196,000/= kutoka kwa Mzabuni PKM Service Station

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/12:KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA MATAIRI 5 IDARA YA AFYA KWA AJILI YA GARI LA WAGONJWA (AMBULANCE)**

Wajumbe walijulishwa kuhusu maombi ya idara ya Afya ya kununuliwa matairi 5 ya gari la wagonjwa.Nukuu za bei zilitolewa na wazabuni walijaza bei kama ifuatavyo:-

| Na. | JINA LA MZABUNI | BEI YA MZABUNI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Amos C.Mkami | 3,900,000 |
| 2 | Magutu Auto Parts | 4,250,000 |

Scanned with CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Nahima Auto Parts | 4,000,000 |

Wajumbe wa bodi ya zabuni walijadili nukuu hizo za bei na kuidhinisha Mzabuni Amos C. Mkami kuiuzia Halmashauri matairi 5 kwa gharama ya Tzs 3,900,000/=

**MUH NA.HMT/BZ/02/03/2022/13:KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni alifunga kikao saa 10:00 mchana baada ya mjadala mrefu lakini wenye tija kwa Halmashauri.

Umesainiwa tarehe 27/04/2022

Fredrick K.Juma

Saini..........................................

Mwenyekiti

Damian Morice Ogila

Saini..........................

Katibu

Scanned with CamScanner